

Pitisha vyuma viwili mbele kisha ufungue vyuma vya juu au fremu huku ukiacha sehemu kubwa ya kufanyia kazi huku ukielekeza moshi polepole upande huo ili nyuki wasalie ndani ya mzinga huku ukiendelea kufanya kazi. Zingatia miondoko ya polepole. Miondoko ya haraka huwakasirisha nyuki. Chunga kuwaangamiza nyuki.

#### vi) Utoaji wa asali

Toa sega zilizojaa kabisa au thuluthi mbili ( $\frac{2}{3}$ ) ili kupata asali ya chini ya asilimia 20 ya unyevu. Usitoe sega ambazo zina makinda au charua maana hupunguza kiwango cha uzuri wa asali.

#### vii) Kutayarisha asali

Kutayarisha kwa kiwango kidogo kunafanywa kwa kutumia ala za nyumbani. Vunja sega zilizochaguliwa kisha uipitisha mseto huo kwenye vichunji kadhaa (mashimo 60, 90 na 120 kwa ichi moja mraba) kwa mpito wa kipepekee kwa muda wa massa 12. Usifinyilie.

#### viii) Kupakia asali

Pakia asali katika chupa au mifuko ya plastiki tayari kuuza. Asali yaweza kuuzwa ikiwa segani kabla ya kutayarishwa. (Asali ya segani).



### Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

#### Mtayarishaji:

Munga, G.S

#### Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

#### Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Mtwapa

S.L.P. 16, Mtwapa

Simu/nukulishi: 0202024751

Baruapepe: karimtw@kari.org

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 59 /2008

**Shilingi Ishirini za Kenya**

## Uwekaji wa nyuki pwani ya Kenya



## Utangulizi

Kilimo cha asali ni njia nyingine ya kujipatia pato katika pwani ya Kenya. Mahitaji mengi ya matokeo ya mizinga ya nyuki ya hali ya juu yanahitaji matumizi ya mbinu za kisasa za uwekaji nyuki.

Hatua zifuatazo zinaweza kuzingatiwa kuongezea mapato ya asili.

### i) Kutayarisha mahali pa kuweka mizinga

- Iweke mizinga kwenye kivuli, mbali na miale ya jua kwa kuwa joto jingi huharibu sega la nyuki.
- Tengeneza mahali hapo takribani mita 100 kutoka kwa nyumba iliyo karibu sana.
  - Kuza ua kuzunguka mahali hapo ili nyuki waruke juu wanapotoka au kurudi mahali hapo.
  - Wawekee maji ili kusitisha uhasama wao nyumbani.

### ii) Tumia mizinga ya kisasa

Mizinga ya kisasa ina vifuniko vinavyoweza kuondolewa vinavyoruhusu kufunguliwa ili kuchunga mienendo ya nyuki bila ya kuwaathiri.

- Weka bodi ngumu chini ya mlango wa bati ili kuzuia joto jingi na nyuki wapate makao mema.
- Katika kujenga mizinga, tumia miti isiyoharibiwa na mchwa, isiyooza haraka kutokana na athari za jua, mvua, kukunjika au isiyoothiriwa na nyuki, kwa mfano mti wa mvule.

### iii) Kuwakinga wadudu

Wadudu wanaotisha makao ya nyuki na kukuzwa kwa makundi yao ni pamoja na nta,



Mahali ya kuweka mzinga

nondo, chungu au mchwa wavamizi wa nyuki, buibui na kuchakuro.

- Hifadhi makundi yenye afya ili kuwakinga wavamizi.
- Ikague mizinga kila mwezi ili kuondoa utando wa buibui na wanyama wagugumaji/kuchakuro.
- Dumisha usafi wa mahali pa mizinga.
- Paka dawa iliyochanganywa na mafuta ya glisi kwenye nyaya za kuning'iniza.

### v) Kuwashughulikia nyuki

#### a) Mavazi yanayostahili

Mavazi ya kujikinga yanahitajika wakati wa kuwashughulikia nyuki. Mavazi hayo yahahusisha:-

- Mavazi maalum ya nyuki pamoja na kofia, glavu za ngozi, pamoja na viatu vya buti vya mpira.
- Ala hizo zingine ni pamoja na kifaa cha kupulizia moshi, ala za mizinga na brashi ya nyuki. Muulize mfanyikazi mwenziyo ikiwa umevaa vilivyo kabla ya kuingia mahali pa mizinga.

#### b) Kuanzisha moshi

Ili kupunguza ukali wa nyuki, kuzipuliza moshi kufanywe kwa moshi laini wa majani makavu, masalio ya miti au unga wa mbao.

- Washa moto kuanzia shinani kisha usheheni kwa malighafi za moto (mafuta) kuanzia juu kisha ufinyilie mpaka ala ijae kabisa.
- Tilia hewa mara kadha hadi kuwe na moshi unaoashiria kwamba moto u tayari kabla ya kufunga kifuniko. Ala hiyo ya moshi iko tayari kutumiwa sasa.



Kifaa cha moshi

#### c) Kuufungwa mzinga

- Jiepushe kuukabili mlango wa mzinga wa nyuki moja kwa moja kwani kuwazuia nyuki katika msafara wao wa kuruka huwafanya wawe wakali zaidi. Puliza moshi kuanzia mlango na kando kando ya kifuniko kisha usuburi kwa muda wa dakika mbili kisha urudie tena kabla ya kuufungua.

Kifuniko kikiwa kimefunguliwa, gonga pole pole vyuma vya juu au fremu kuanzia mbele kurudi nyumba ili kutambua kiwango cha sega kilichoengwa. Pale patakapokuwa na mabadiliko ya sauti panamaanisha mwisho wa sega.